TANGAZO LA SERIKALI Na. 399 la tarehe 26 Desemba

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

SURA YA 287

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya vifungu cha 153

## SHERIA NDOGO ZA (KUFUFUA NA KUTUNZA MASHAMBA YA KOROSHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA, 2008

Jina na mwanzo wa kutumika

1 Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kufufua na Kutunza Mashamba ya Korosho) za Halmashauri ya wilaya ya Kyela na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

Matumizi

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya wilaya ya Kyela.

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa Kilimo na mifugo pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya wilaya ya Kyela.

"Magugu" maana yake ni mimea ambayo huota na kuathiri ukuaji au ustawi wa mikorosho.

"Mbegu Bora" maana yake ni mbegu zinazozalishwa na vituo vya uzalishaji wa mbegu za zao la korosho vilivyoko chini ya kituo cha utafiti wa kilimo Mtwara

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Kyela pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekelza majukumu ya Mkurugenzi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Wajibu wa kulima shamba la korosho | 4 | (1) | Ni wajibu wa kila mkazi wa Halmashuri mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea kulima Shamba la korosho lenye ukubwa wa ekari mbili kwa kutumia mbegu bora. |
| | | (2) | Ni wajibu wa kila mmiliki wa shamba la korosho kutunza shamba hilo na kupalilia magugu kwa kutumia dawa za kuzuia au kutibu magonjwa mbalimbali kama itakavyoshauriwa na Afisa Muidhiniwa. |
| | | (3) | Kila Afisa mtendaji wa kata atakua na wajibu wa kutunza kumbukumbu na kusimamia utunzaji wa mashamba yote ya korosho yaliyoko kwenye kata yake. |
| Udhibiti wa magonjwa | 5 | | Ni wajibu wa kila Mmiliki wa shamba la korosho kutoa taarifa kwa Afisa Muidhiniwa endapo shamba lake limeingiliwa na wadudu au magonjwa ili kuzuia uenezaji wa magonjwa au wadudu kwenye mashamba mengine. |
| Uwezo wa Afisa muidhiniwa | 6 | | Afisa Muidhiniwa anaweza kwa wakati wowote kuingia shambani kukagua hali ya shamba na ustawi wa korosho. |
| Uvunaji wa korosho | 7 | (1) | Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuna korosho kwa kuangusha. |
| | | (2) | Uvunaji wa korosho ni ule wa kuokota tunda la korosho ambalo limeanguka lenyewe baada ya kukomaa. |

(3) Baada ya kuokota matunda ya korosho yaliyokomaa mkulima atatenganisha korosho na tunda na anapaswa kukausha korosho hizo juani kwa kutumia vifaa visafi.

(4) Baada ya korosho kukauka mkulima atatenga korosho zake katika daraja la kwanza na daraja la pili na kuzihifadhi kwenye magunia ya mkonge.

Uhifadhi wa korosho

8 (1) Ni marufuku kwa mkulima yeyote kuhifadhi Korosho kwenye vifaa visivyopitisha hewa kama mifuko ya plastiki au viroba.

(2) Korosho zilizohifadhiwa kwenye magunia zihifadhiwe kwenye maghala yenye sifa zifuatazo:-

- (i) Linaloingiza hewa ya kutosha
- (ii) Lisilopitisha maji
- (iii) Lenye reli ya kubeba magunia ya korosho (pallets)

Uuzaji wa korosho

9 (1) Mkulima wa Korosho atapaswa kuuza korosho zake kwenye kituo cha kuuzia Korosho kilichosajiliwa na Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushauriwa na Halmashauri.

(2) Mkulima atauza Korosho kwa mnunuzi mwenye leseni iliyotolewa na Bodi ya korosho pamoja na kibali atakachopewa na Halmashauri

(3) (i) Kibali kitakachotolewa na Halmashauri kitakuwa cha tani 100 na kitaonyesha:-

- (a) Jina kamili na anuani ya posta
- (b) Mahali ilipo ofisi na namba ya simu
- (c) Kiasi cha tani zinazonunuliwa au zilizonunuliwa pamoja na namba ya stakabadhi iliyolipiwa ushuru

(ii) Baada ya tani 100 kuisha mnunuzi atalazimika kulipa ushuru wa kiasi kilichozidi na kuomba kibali kingine

**Muda wa kuuza na kusafirisha korosho**

10 (1) Ununuzi na usafirishaji wa korosho utafanyika kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni

(2) Kila mnunuzi wa korosho atatakiwa kusafirisha korosho alizonunua akiwa na nyaraka muhimu ambazo ni kibali cha kununulia na kusafirishia mazao kilichotolewa na Halmashauri, PDN na CBT.

**Wajibu wa mnunuzi**

11 Mnunuzi wa Korosho atakuwa na wajibu wa:-

(i) Kutumia kapani iliyokaguliwa na Maafisa vipimo kabla ya msimu wa ununuzi kuanza.

(ii) Kununua Korosho kwa mkulima aliyesajiliwa kwa kunakili namba ya mkulima huyo (GRN)

(iii) Kuweka kumbukumbu sahihi za ununuzi wa korosho kadri itakavyohitajika na Bodi ya Korosho Tanzania au Halmashauri.

**Makosa na adhabu**

12 Mtu yeyote ambaye:-

(i) atashindwa kutekeleza ushauri aliopewa na Afisa Muidhiniwa katika kutunza Shamba lake

(ii) atashindwa kutoa taarifa ya wadudu au magonjwa yaliyoingia shambani kwake

(iii) atanunua au kusafirisha korosho wakati wa usiku

(iv) atampa mtu mwingine kibali chake

(v) atanunua korosho bila kuwa na leseni ya biashara pamoja na kibali cha Halmashauri

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ulibandikwa kwenye sheria hizi ndogo kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 24/5/2008 Muhuri huo ulibandikwa mbele ya

T.M KISUGUJILA
MWENYEKITI WA HALMASHAURI

M.H. SENYAGWA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)

NAKUBALI

DODOMA

**MH. MIZENGO K. PETER PINDA (MB)**
**WAZIRI MKUU**

TAREHE 31/10/2008